# TABIA YA YUSUFU

## Mafundisho maalumu kwa watoto



Mch. Denis & Devis Julius
https://wingulamashahidi.org/

# MAFUNDISHO MAALUMU YA WATOTO.

## UTANGULIZI.

Huu ni mfufulizo wa mafundisho maalumu ya Watoto umri 0-12. Miongozo hii inaandaliwa na Kanisa la Nuru ya Upendo wa Kristo. Ikiwa utapenda kupata miongozo ya madarasa ya nyuma, mwisho wa Makala hii utapata mawasiliano.  Ikiwa pia una shuhuda au ufadhili, mawasiliano ni hayo hiyo.

Katika fundisho hili, wewe kama mzazi utajua mambo muhimu unayopaswa uyajenge kwa mtoto tangu akiwa mdogo, ili yale yaliyoingia ndani yake, aidha kutoka kwa Mungu, mwanadamu au shetani, yadhihirike nje, Uweze kumsaidia kusimama na kuishi vema katika maisha ambayo Mungu amemkusudia aishi duniani. Mwongozi huu umeegemea hasaa katika maisha ya Yusufu, ambapo ndani yake lipo fundisho kubwa sana. Hivyo wewe kama Mwalimu/mzazi, ili uweze kuwajengwa vema Watoto uwafundishao, chukua muda wako binafsi omba, kisha Soma kitabu cha Mwanzo kuanzia sura ya 37-51. Hapo utaelewa kwa undani maisha yote ya Yusufu, kwasababu mwongozo huu utakuhitaji uwasimulie kwa lugha rahisi Watoto, Habari ya maisha yake.

~ Mchungaji Denis & Devis Julius.

# TABIA YA YUSUFU.

*Mwanzo 37:1Yakobo akakaa katika nchi aliyosafiri baba yake, katika nchi ya Kanaani.*
*[2] Hivi ndivyo vizazi vya Yakobo. Yusufu, aliyekuwa mwenye miaka kumi na saba, alikuwa akichunga kondoo pamoja na ndugu zake; naye alikuwa kijana pamoja na wana wa Bilha, na wana wa Zilpa, wake wa baba yake. YUSUFU AKAMLETEA BABA YAO HABARI ZAO MBAYA.*
*[3] Basi Israeli akampenda Yusufu kuliko wanawe wote, maana ni mwana wa uzee wake, akamfanyia kanzu ndefu.*

Kilichomfanya Yusufu kupendwa na wazazi wake, lakini pia awe mkuu sana, na zaidi ya yote, Kupata kibali kikubwa machoni pa Mungu, ni tabia yake aliyoionyesha tokea akiwa mtoto. Na tabia yenyewe, ni KUWA MUWAZO WA MAMBO YOTE.

Yusufu alipoona, uovu hakuufumbia macho, Yusufu alipoona hata ndoto zisizoeleweka machoni pake hakuzificha, alizieleza kwa wazazi wake wazi wazi, Hii ilionekana kama hulka, lakini ilimsaidia sana, na ndio iliyomfanya shetani asiwe mwepesi kumweza na awe mkuu.

Yusufu alipoona ndugu zake wanatukana, haraka sana alikwenda kumwambia baba yao, alipowaona wanasema uongo, wanaiba, moja kwa moja aliripoti taarifa zao haraka sana kwa wazazi wake. Ijapokuwa ilimgharimu kuchukiwa lakini huo ndio ulikuwa ufunguo wa mafanikio yake makubwa ya tabia.

Hata sasa, kama wazazi/ walezi tukiijua siri hii, tataanza kuwajengea Watoto wetu mapema tabia hii ya KUWA WAWAZI WA MAMBO YAO YOTE. Na matokeo yake kuwalinda na yule mwovu.

Ushindi mkubwa wa shetani kwa Watoto, ni kuwafanya wafiche mambo yao, au kuwa na vitu wavijuavyo wao tu, sirini peke yao, ili aendelee kuwaangamiza kimya kimya rohoni. Ni lazima tufahamu kuwa kwa mtoto SIRI haimjengi, bali ina muangamiza, Na Watoto wengi wanamekuwa wasiri, hali ambayo imeathiri hali zao za kiroho hadi kimwili.

Na hiyo imechangiwa aidha na hofu ya kuadhibiwa na wazazi au kukemewa, pale wanapozungumza. Hivyo shule hii, ni namna ya kumwandaa mtoto, kuwa muwazi, ili kumsaidia mzazi/ mlezi, kutambua kilicho ndani yao, kama ni cha Mungu au cha shetani.

Lakini pia kumwelimisha mzazi, kuweka mazingira mazuri ya mtoto kuwa huru kusema mambo yake.

## MWANZO:

Awali ya yote tumia lugha nyepesi sana, kuwasimulia Habari ya Yusufu, tangu akiwa mdogo, mpaka alipochukiwa na ndugu zake na kuuzwa utumwani, kisa alikuwa akifichua mambo yao maovu hadharani, na kueleza yaliyoendelea moyoni mwake wa uwazi, waeleze jinsi alivyokuwa mwaminifu mpaka kufungwa gerezani, lakini hakuacha kumpenda Mungu, na hatimaye, Mungu akaenda kumfanya kiongozi mkubwa katika taifa la Misri, (Mwanzo 37-50)

Kisha waulize, ni wangapi hapa wanataka kuwa kama Yusufu?

Watanyoosha mikono: Ndipo uanze kuwaeleza hatua ambazo wanapaswa wazichukue. Ili wapendwe na wazazi wao kama Yusufu Pamoja na Mungu.

**Yafuatayo ni maeneo ambayo unapaswa umfundishe mtoto, kuyaweka bayana.**

I. MARAFIKI (WATOTO WENZAKE):

Wafundishe, ikiwa watasema maneno yasiyofaa kama vile matusi. Moja kwa moja bila kukawia amtafute Mwalimu/mzazi/ amweleze tabia zao . Asikae kimya.

Zoezi: Unaweza kumuuliza/kuwauliza je! Kuna kitu gani kibaya, wamekisikia kwa wenzao, siku ya leo, au hivi karibuni. (wakunong'oneze kila mmoja jambo lao)

Ndipo Atasema/ Watasema baadhi, lakini pia wengine wataogopa kusema: Kisha wapongeze wale waliosema kwa uwazi

Kisha waambie wote nyie mtakuwa kama Yusufu, mnavyokuwa wawazi hivi hivi. Baada yah apo wafundishe sasa, kwa upole madhara ya kusikia maneno mabaya kwamba yatawaharibu tabia zao.

Wafundishe kukariri kifungu hichi:

1Wakorintho 15:33

*[33] Msidanganyike; Mazungumzo mabaya huharibu tabia njema.*

Zaburi 1:1-2

*Heri mtu yule asiyekwenda Katika shauri la wasio haki; Wala hakusimama katika njia ya wakosaji; Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha.*
*[2] Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku*

Hili funzo wakilielewa vizuri, watajilinda na tabia za kipepo tokea wakiwa wadogo, tukifahamu kuwa shetani hutumia kampani ovu, kufundisha uovu. Watoto wengi huharibikiwa wakiwa na Watoto wenzao, wala sio kutoka kwa watu wazima.

2. MWILI WAKE.

Wafundishe Watoto, wanapoona, kuna mtu yoyote, au mmojawao anataka kumshika au kutazama maeneo yake ya sirini, au anaonyesha dalili zozote za namna hiyo, haraka sana akimbie, na kisha akatoe taarifa hiyo kwa mzazi, bila kukawia. Waeleze Yusufu alipoona tabia hizo kwa mke wa Potifa alikimbia mbio, na wao pia wasikawie kukimbia.

Wafundishe uwaambie miili yao ya hekalu la Roho Mtakatifu, hivyo mtu yeyote hataugusa.

Wakaririshe kifungu hichi:

1Wakorintho 3:16

*[16] Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?*

3. NDOTO ZAKE:

Wazazi wengi, hawajui ndoto, ni langu kubwa sana la Watoto, Na kwa kujua ndoto zao unaweza kuzielewa hisia zao, unaweza kuelewa mashambulizi ya shetani, unaweza kuelewa ujumbe wa ki-Mungu ulio juu yao. Yusufu alikuwa anaota ndoto, lakini hawakutaka kutilia maanani, zilipokuja kuwa kweli ndipo walipotambua aliyowaambia.

Sasa wewe kama mazazi/ Mlezi.

Waulize mmoja mmoja: Ni ndoto gani nzuri walizoota wanazozikumbuka

Ndoto gani mbaya walizoota wanazikumbuka

Kisha mwishoni wape uhuru kwa kusema ndoto zozote walizoota.

Kisha watie moyo kwa kuwaambia, hongereni kwa kuwa mmekuwa kama Yusufu, kueleza ndoto zenu.

Ukweli ni kwamba utasikia mengi, ambayo mengine yatahitaji maombi. Kwamfano wapo Watoto ambao, wachawi wanawajia usiku, na kuwapeleka vilingeni na wanakemewa wasizungumze chochote, ikiwa watafanya hivyo watauliwa (shuhuda za namna hiyo ni nyingi sana), wengine mapepo yanawatokea na kuwakaba.. Hivyo akikaa kimya ndivyo uharibifu wao unavyoongezeka.

Lakini kuna Watoto wengine ni manabii tangu kuzaliwa kwao, ndoto zao huwa kweli, uwasikilizapo utatambua kusudi la Mungu juu ya maisha yao, lakini pia juu ya watu wote.

Yeremia alikuwa ni mtoto, lakini Mungu alimtumia kutoa tabiri kwa mataifa. Kamwe usipuuzie malango ya ndoto ya Watoto.

Hivyo wewe kama Mwalimu/mzazi, zidi kuwasisitiza sana, Mungu anapendezwa na Watoto wawazi, na hao ndio watakaofanikiwa.

4. KUKOSEA/ KUTENDA DHAMBI

Wafundishe kuomba msamaha: Pale wanapokosea haraka sana, wasikae kimya, bali waende kueleza makosa yao kwa wazazi, kisha wazazi watawasamehe.

Ikiwa walifanya kitendo chochote cha wizi, waeleze, amri ya Mungu inasema usiibe. Waende haraka sana kuwaeleza wazazi wao makosa yao, kisha waombe msamaha, na wasiibe tena.

Ikiwa wamepigana: Wafundishe, Kuepuka tabia hizo, na haraka wawaeleze waalimu, au wakubwa zao, wasikae kimya, ili wasaidiwe kupatanishwa, vitendo hivyo visijirudie tena.

Waambie kitendo cha kuomba msamaha ni chema na watapendwa na watu.

Halikadhalika, wanapojiona wana hofu, au woga, wa kitu fulani, au mtu, au ndugu, waambie, wazungumze kwa wazazi wao, wasikae kimya.

5. UHURU WA KUJIELEZA.

Wewe kama mzazi/ Mlezi, Mpe nafasi Kila mtoto, kila siku, asimulie, hadithi yake anayoijua katika biblia, kile alichofundishwa kwenye kipindi cha dini shuleni, au jambo lolote kuhusu Mungu kisha, tumia nafasi Hiyo kumtia moyo, na kumsaidia uelewa bora, hiyo itasaidia, kumlinda mtoto na udanganyifu wa mafundisho potofu tokea wakiwa wadogo.

Kumbuka Imani huja kwa kusikia, usipuuzie mambo ya kiroho mtoto wako ayasikiayo huko nje.

## MITANDAO, SIMU, & LUNINGA

Hatuwezi kukataa uhalisia uliopo sasa, kwamba simu, Internet, luninga, ni vitu vinavyoiendesha dunia sasa na haviepukiki popote, vimekuwa msaada mkubwa kwa wanadamu, lakini pia vimekuwa sumu kubwa sana ya mwanadamu pale vinapotumika kinyume.

Na kwa Bahati mbaya makundi ya Watoto, katika karne hii ya 21, yameathirika pakubwa, kiasi cha kupoteza maadili, kama sio kuzama katika matendo ya giza kabisa, Hiyo yote ni kwasababu wazazi kushindwa kuwadhibiti mapema tokea wakiwa wadogo.

Mara nyingi pale inapokuwa ngumu kuwazuia, walezi hutumia katazo la nguvu, na matokeo yake, wanaacha kutazama hadharani, wanahamia sirini. Na hiyo ni mbaya sana.. Pamoja na kwamba zipo nyakati katazo la nguvu linahitajika, lakini pia, Kuelekezwa, na kufundishwa madhara ya vitu hivyo kunapaswa kutangulie kwanza.

Mtoto akifundishwa sana ubaya wa kitu, zaidi ya kukatazwa tu, humjengea tahadhari kubwa sana ndani yake, hata wakati ambapo wazazi hawamchungi, kwasababu yeye mwenyewe anajua ninakwenda kujiangamiza mwenyewe. Tumia muda mwingi, kumweleza hatari ya simu, kuliko kumkemea kutumia simu.

Unawafundishaje?

Waambie, Tv, na simu, na upakuaji, usioelekezwa na wazazi ni hatari kwa maisha yao ya kiroho. Na vina haribu akili zao. (waambie shetani pia yupo kwenye mitandao, Tv, magemu na Simu) ili kuwaangamiza na kuwapeleka motoni. Wakijua uhalisia huu ni msingi mzuri sana.

Wafundishe kukiri: 'Sitapakua chochote mtandaoni, bila idhini ya wazazi wangu'.

Wakiri tena: 'Nitakuwa tayari, kusema kila kitu nikionacho kwa wazazi wangu'

Wakiri tena: 'Nitawatii wazazi wangu pale wanaponikataza kutazama, simu au Tv'.

Kama mzazi watengenezee njia: Nyepesi kuwa kuwapakulia, video ambazo zipo tayari za mafundisho ya Watoto, sauti za biblia, vipindi vya masomo ya darasani, video za hadithi za biblia, hata wakiangalia tv, waruhusu kwa muda stahiki, na kwa kiasi, ziwe chaneli zenye staha za Wanyama, au zenye maudhi ya kuwajenga.. epuka kuwaacha Watoto kwenye kipindi/ tamthilia zozote zile, au Filamu, epuka kuwapa uhuru wa kupakua you-tube wao wenyewe bila uangalizi. Dunia ya sasa imeharibikia mtandaoni, usimpe mwanao simu, mpe kitabu, ni heri ukacheze naye nje, kuliko kucheza naye kwenye simu na magemu.

Hitimisho.

Mambo haya mawili yakizingatiwa yaani, mtoto kujengewa ujasiri wa "Kuweka wazi mambo yake ya siri" lakini pia "kudhibitiwa uhuru wake wa kimitandao kimikakati" Kwa sehemu kubwa sana, shetani atakuwa ameshindwa vita dhiki ya Watoto wetu. Tuwapende Watoto wetu, tuwajenge Watoto wetu.

Mithali 22:6

*6 Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee*

## MAWASILIANO

Kanisa la Nuru ya Upendo

Namba za Wachungaji: +255693036618 / +2557890011312

Email: info@wingulamashahidi.org

Website: https://wingulamashahidi.org/